“Hajawahi Kunena Mwanadamu Kama Anenavyo Mtu Huyu”

(Never Man Spake Like This Man”)

Na

Ellis P. Forsman

“Hajawahi Kunena Mwanadamu Kama Anenavyo Mtu Huyu”

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 13, 2011

“Hajawahi Kunena Mwanadamu Kama Anenavyo Mtu Huyu”

Yohana 7:43-46

Ni nani assiyevutiwa katika kusikiliza maneno ya watu wakuu?

Yapo maneno mazuri yaliyoandikwa kwenye Biblia na watu wakuu wa Mungu. Lakini maneno ya Yesu yalikuwa na ladha tofauti ukilinganisha na zingine.

Tukio la fungu la maandiko:

Yohan 7:32, “*Mafarisayo wakawasikia makutano wakinung’unika hivi juu yake basi wakuu wa makuhani na Mafarisayo wakatuma watumishi ili wamkamate.*”

Wakuu wa makuhani waliuliza. Yoh. 7:45, “*Basi wale watumishi wakawaendea wakuu wa makuhani na Mafarisayo. Nao wakawaambia mbona hamkumleta?*”

Jibu la watumishi. Yoh. 7:46, “*Hajanena kamwe mtu yeyote kama huyu anavyonena.*”

Hotuba ya Yesu ilijumuisha nini?

Haikuwa:

- Kwa sababu ya mavazi yake ya mtindo.
- Kwa sababu ya uzuri wake wa mwili. Isa. 53:2, “*Maana alikuwa mbele zake kama mche mwororo, na kama mzizi katika nchi kavu; yeye hana umbo wala uzuri; na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani.*”
- Kwa sababu ya elimu yake. Yoh. 7:15, “*Wayahudi wakastaajabu wakisema, amepataje huyu kujua elimu, ambaye hakusoma?*”

- Kwa sababu alikuwa mtu mwema.

Ni kwa sababu Yesu alikuwa na cha kusema na alilisema.

Hajawahi kunena mtu yeyote kama huyu:

Kwa mamlaka hayo ya kipekee.

Mat. 7:29, "*Kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao.*"

Katika hotuba ya mlimani yote, Yesu alisema, "*Imenenwa,…lakini mimi nawaambia.*"

- Mat. 28:18, "*Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani*."
- Efe. 1:22-23, "*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya <u>vitu vyote kwa ajili ya kanisa</u> ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anaye kamiliska kwa vyote katika vyote.*"

Lakini Yesu asingebaki duniani milele; hivyo basi, mtu anayamfuata alipaswa kuja na kuongea kwa mamlaka.

Hivyo, Yesu akawafundisha mitume wake kwa zaidi ya miaka mitatu katika injili ya ufalme wake unaokuja; alafu aliwahidi Roho Mtakatifu kuwaongoza katika ufunuo na maandishi ya jumla ya mapenzi yake.

- Yoh. 16:13, "*Lakini yeye atakapokuja huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari zake.*"
- 1 Kor. 2:12-13, "*Lakini sisi <u>hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu</u> makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. <u>Nayo twayanena</u>, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni*."

Wapo wale wanaaoishi wakati wa Paulo ambao hawakutaka kukubali kile alichosema kwa sababu alilitesa kanisa. Wapo wale wanaoishi leo ambao hawakubali alichosema Paulo kwa sababu wanasema aliwachukia wanawake.

1 Kor. 14:37, "*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba <u>ni</u> maagizo ya Bwana.*"

Lakini Paulo hakunena yaliyoyake mwenyewe, bali kama alivyoongozwa na Yesu Kristo kupitia Roho Mtakatifu.

Kwa vile Paulo na mitume wote walinena kwa mamlaka; pia waliandika kwa mamlaka.

Lakini vipi kuhusu leo? Wakati wowote mhubiri wa injili anapolifungua neno la Mungu na neno likasomwa kutoka kwenye kitabu, na inaonyeshwa, kufundishwa, kuongelewa, kuwasihi watu ili waiamini, inaweza kufanyika kwa mamlaka. Siyo kwa mamlaka ya mhubiri, bali kwa mamlaka ya neno la Mungu.

Sina mamlaka binafsi, hakuna mhubiri yeyote wa injili aliye na mamlaka yake binafsi, alafu tunaweza kwa mamlaka. Kivipi? Kwa kuthibitisha kwamba neno tunalohubiri ni neno la Mungu.

- 2 Tim. 4:3-4, "*Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.*"
- 1 Pet. 4:11, "*Mtu akisema na asema kama mausia ya Mungu…*"

Kwa faida kama hiyo ya uungu.

Neno lake lilishikilia bahari, iliyoonyesha uwezo wake juu ya asili. Mat. 8:26-27, "*Akawaambia mbona mmekuwa waoga enyi wa imani haba? Mara akaondoka akazikemea pepo na bahari kukawa shwari kuu. Wale watu wakamaka wakisema huyu ni mtu wa namna gani hata pepo zza bahari zamtii?*"

Neno lake liliwapa mwanga vipofu, viziwi wanasikiaa, mabubu wanaongea, na kuwapa nguvu vilema kutembea, hivyo kuonyesha uwezo wake juu.

Neno lake linanena msamaha wa dhambi, hivyo kuonyesha uwezo wake juu ya dhambi.

Neno lake liliwafufua wafu kutoka makaburini, hivyo kuonyesha uwezo wake juu ya kifo. Yohana 11:43-44, "*Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro njoo huku nje. Akatoka nje yule aliyekufa, akafungwa sanda miguuni na mikononi, na uso wake amefungwa leso. Naye Yesu akawaambia, mfungueni mmwache aende zake.*"

Kwa urahisi wa ajabu kama huo.

Alitumia meneo, kauli, naa mifano ili watu waelewe.

Marko 12:37, "*…Walikuwa wakimsikiliza kwa furaha.*"

Injili ni kitu rahisi na inapaswa kunenwa kwa maneno rahisi.

Miaka mingi mara iliyopita ndugu kijana alikwenda kumrekebisha mhubiri mzee kwa kitu alichokisema na kupata karipio kali. "Usinirekebishe. Nina ujuzi katika Biblia."

Isa. 35:8, "*Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia nayo itaitwa, Njia ya utakatifu wasio safi hawatapita juu yake; bali itakuwa kwa ajili ya watu hao, wasafirio, wajapokuwa wajinga,hawatapotea katika njia hiyo.*"

Wajinga – hawana mawazo mazuri; sio werevu.

Kwa ujasiri kama huo.

Pia alinena kwa ujasiri.

- Mat. 21:12-13, "*Yesu akaingia ndani ya hekalu akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni, akzipindua meza za wabadili fedha na viti vyaao waliokuwa wakiuza njiwa; akawaambia imeandikwa nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi.*"
- Mat. 23:14, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnakula nyumba za wajane, na kwa unafiki mnasali sala ndefu; kwa hiyo mtapata hukumu iliyo kubwa zaidi.*"
- Alidai kuwa na Baba kabla ya ulimwengu kuumbwa.
- Yoh. 1:1-3, "*Hapo mwanzo kulikuwako neno naye neno alikuwako kwa Mungu naye neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwa kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika.*"
- Yoh. 17:5, "*Na sasa Baba unitukuze mimi pamoja nawe kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako.*"

Siyo tu alidai kuwa Mwana wa Mungu, lakini pia akawa sawa na Mungu. Fil. 2:6, "*Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu,…*"

Ya wokovu.

Yohana 3:14-16, "*Na kama vile Musa alivyomuinuaa yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata kamatoa Mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.*"

Paulo alitumia maneno sahihi alipoita "*wokovu mkuu.*" Heb. 2:3, "*Sisi je tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale walio sikia.*"

Kwa nini ni wokovu mkuu

Kwa sababu ya gharama yake. 1 Pet. 1:18-20, "*Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwanakondoo asiye na hila, asiye na waa, yaani Kristo. Naye amejulikana kweli tangu zamani kabla haijawekwa misingi ya dunia; lakini alifunuliwa mwisho wa zamani kwa ajili yenu.*"

Kwa sababu ya upana wake.

- Rum. 3:23, "*Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*"
- Yoh. 3:16, "*Kwa jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanaye wa pekee ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.*"

Kwa sababu ni wokovu war oho. 1 Pet. 1:9, "*Mkiupokea mwisho wa imani yenu hata wokovu wa roho zenu.*"

Kwa sababu ya uzima uliopo ngambo ya kaburi.

Kwa sababu Kristo alikuja kwa wanadamu, ilikuwa ikiuliza swali, kama ilivyoandikwa katika Ayubu 14:14, "*Je mwanadamu akifa, ataishi tena?...*"

Baada ya Kristo kuja na kufa kwa ajili ya dhambi zetu, na akafufuka kutoka katika wafu, hivyo wanadamu wanaweza kuthibitishiwa uzima baana ya kufa.

- Yohana 10:10, "*Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.*"
- Yohana 14:1-3, "*Msifadhaike mioyoni mwenu mnaamwamini Mungu niaminini na mimi. Nyumabni mwa Baba yangu mna makao mengi kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali; nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo.*"

Yesu alisema hakujua mwissho wa nyakati ungekuwa ni lini, lakini kwamba neno lake litadumu milele. Mat. 24:35, "*Mbingu na nchi zitapita lakini maneno yangu hayatapita kamwe. Lakini kuhusu siku hiyo na saa hakuna aijuaye, hata malaika wa mbinguni bali Baba pekee.*"

Je umewahi kujiuliza ni kwa nini kanisa ni dogo? Kuna sababu nyingi juu ya hili. Inakatisha tamaa tunapoona idadi ya watu hushuka, lakini Yesu alisema itakuwa hivyo atakaporudi. Luka 18:7-8, "*Na Mungu je hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku, naye ni mvumilivu kwao? Nawaambia atawapatia haki upesi; walakini atakapokuja Mwana wa Adamu, je ataiona imani duniani?*"

Kamusi ya Coffman: "…kanisa, katika nyakati za mwisho, litapungua hata katika masalia machache…"

Kwa nini Yesu alinena kuliko mtu yeyote?

Kwa sababu Mungu alikuwa ananena kwa niaba yake; alikuwa Emanueli; alikuwa Mungu pamoja nasi.

- Yohana 14:24, "*Mtu asiyenipenda, yeye hayashiki maneno yangu; nalo neno mnalolisikia silo langu, ila ni lake Baba aliyenipeleka.*"
- Heb. 1:1-3, "*Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana,*

aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufaanya ulimwengu. Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;"

Hivyo, ndiye njia pekee ya kwenda kwa Baba.

- Yohana 14:6, "*Yesu akamwambaia mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"
- 1 Tim. 2:5, "*Kwa sababu Mungu ni mmoja na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu.*"

Hitimisho

Tutahukumiwa kwa kile alichosema Yesu.

Yohana 12:48, "*Yeye anikataaye mimi, asiyekubali maneno yangu anaye amuhukumuye nano hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho.*"

Je unaweza kumsikiliza na kutii sauti yake leo? Ameshatuambia namna ya kufanyika Wakristo. Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6*, "Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38*, "Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

  Matend 11:18*, ".....Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima."</u>*

Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, “Kwamba kuna mwizi!” taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, “samahani; samahani!” Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10*, “Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.”*

Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni “**KATIKA**” haki, uzima, au wokovu. “Katika” inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, *“Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye.”* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, “*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote.”* Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

  Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. *“Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”* (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? “*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*”. Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

  Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. *“Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.”* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena."* (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usifanyike leo?